**Entrepreneurs in Africa – Successful and responsible**

**Episode 6**

**Title: “Believe in yourself” – The Senegalese Artist Ibrahima Mbaye**

**Author: Babou Diallo (Dakar, Senegal)**

**Editor French: Dirke Köpp**

**Proof reading French: Yann Durand and Aude Gensbittel**

**Translator: Salamata Saenger**

**Editors English: Katrin Ogunsade, Adrian Kriesch**

**Proof reading English: Natalie Glanville-Wallis**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

## Characters (O-Töne, clips)/ Narrators

| | Women | Men | Age | Language |
|---|---|---|---|---|
| Intro/Outro | x | X | Unimportant | |
| Narrator | | X | Unimportant | |
| Ibrahima Mbaye Sopey (clip) | | X | about 40 | French |
| Abdoulaye Magued Mouhamed Barry (clip) | | X | About 12 | French |
| Ousmane Ndiaye (clip) | | X | About 25 | French |
| Awa Mbaye (clip) | x | | About 64 | Wolof |
| Ndèye Fatou Mbaye (clip) | x | | About 35 | Wolof |

## Pronounciation [as it would be in German]:

Ibrahima Mbaye Sopey [Ibrahima M-bae Sopeh]

Abdoulaye Magued Mouhamed Barry [Abdulai Maget Muhamed Barry]

Ousmane Ndiaye [Usman Ndiai]

Awa Mbaye [Aua M-bae]

Ndèye Fatou Mbaye [Ndei Fatu M-bae]

Nimzat [Nimsa]

**1. Intro:**

Hujambo na karibu kwa makala nyingine ya “Learning By Ear” Noa Bongo Jenga Maisha yako, tukiwa bado katika mfululizo wa vipindi vyetu kuhusu Wajasirimali waliofaulu katika biashara yao Barani Africa na kuchangia pakubwa maendeleo ya jamii wanamoishi .Leo tunafunga safari hadi nchini Senegal ambako tunagundua siri ya utayarishaji filamu na tunakutana na mkurugenzi mwelekezi wa filamu.

**2. SFX: House of culture Douta Seck**

**3. Narrator:**

Ni Ijumaa mchana tunapowasili katika wiyala ya Medina iliyoko mji mkuu wa Dakar nchini Senegal. Baadhi ya wasanii tayari wanafanya mazoezi katika jumba hili la kutayarisha filamu. Mwelekezi wao ni Ibrahim Mbaye Sopey ambaye sasa anawafunza wasanii mambo ya msingi kuhusu jumba la sanaa.Ukumbi wa mazoezi umefurika wasanii. Vijana wenye hamu ya kushirikishwa katika sanaa hii, wanafuata kwa makini maelezo ya mwelekezi wao. Mchezo wanaofanyia mazozi unahusu tofauti za kikabila na kitamaduni nchini Senegal ambao umeandikwa na Sopey

**4. SFX: More of rehearsal**

**5. Narrator:**

Ibrahima Mbaye Sopey ni msanii, mwigizaji na pia mkurugenzi mwelekezi wa michezo ya kuigiza. Raia huyu wa Senegal ana umri wa miaka 40.Na baada ya kukamilisha masomo yake ya sekondari alijiunga na chuo cha kitaifa cha mafunzo ya usanii mnamo mwaka wa 1994. Miaka mine baadaye Ibrahima alifuzu na kupata cheti chake kabla ya kujiunga na makundi mbali mbali ya usanii. Mnamo mwaka wa 2003 aliamua kuanzisha kampuni yake ya usanii kwa jina "F'Ame" in Woof", na maana ya Woof kwa lugha ya Mama nchini Senegal ni "Kipenzi cha roho ya Mwanamke". Na lengo kubwa lilikuwa kuwakuza kipawa cha wasanii wa Kike nchini humo.

**6. O-Ton: Ibrahima Mbaye Sopey (fr.)**

Wasanii wengi wa kike nchini Senegal hawajulikani. Na nilionelea vyema kuwakuza na kuwapa moyo, kwamba wanayo nafasi ya kufanya vyema zaidi katika ulimwengu wa sanaa nchini Senegal.. Pia ni fursa nzuri kwangu kudhihirisha yote niliyojifunza katika chuo cha sanaa, mbali na kupanua kipawa changu katika sekta hii ya usanii. Ndio sababu nikaamua kuanzisha kampuni."

**7. Narrator:**

Miaka minane baada ya kuanzisha kampuni hiyo ya F'ame, Ibrahima anajivunia ufanisi mkubwa katika kazi anayofanya

**8. O-Ton: Ibrahima Mbaye Sopey (fr.)**

“Kampuni hii ilianzishwa katika mazingira magumu sana. Nilitaka tu kutekeleza yote niliyojifunza chuoni. Kwani nilikuwa na kiu sana kufanya michezo ya kuigiza na pia kuelezea ulimwengu yalimo moyoni mwangu kupitia sanaa.Lakini zaidi kujitafutia riziki maishani mbali na kutoa nafasi za kazi kwa vijana wengine.”

**9. Narrator:**

Hata hivyo lakini haikuwa rahisi kuanzisha biashara hii, kwani kama ilivyo kawaida katika mataifa mengi barani Africa, tatizo kubwa ni mtaji wa kuanzisha biashara anasema Sopey..Sopey alianzisha biashara hii kwa mtaji wa Euro 30 pekee, ambazo alizitumia kama nauli ya wasanii waliokuwa wakishirikiana naye. Kwani hayo ndiyo marupurupu pekee waliyoweza kupata baada ya mazoezi au kutayarisha filamu.Licha ya hali hiyo ngumu, Sopey hakukata tama na alijitolea kutimiza azma yake.

**10. O-Ton: Ibrahima Mbaye Sopey (fr.)**

“Siri kubwa ya ufanisi ni kufanya kazi kwa bidii.Katika chuo nilikosomea masuala ya usanii, nilijifunza mengi jinsi ninavyoweza kupanua kipawa changu na kuwa msanii wa kutambulikana.Tuliweza kujifunza mengi sana lakini pia nikawa na maswali mengi kuhusu sekta hii ‘ Sasa vipi ni kate tama wakati huu’? Hakuna kitu kizuri kama kujiamini wewe mwenyewe. Baada ya masomo kila mmoja alishika njia yake, lakini nilitaka kuwa mfano wa kuigwa.”

**11. Narrator:**

Na kweli Sopey alifuata njia yake. Lakini baada ya miaka kadhaa ya kujitolea kufanya kazi kwa bidii katika kampuni yake, Sopey alipata mtaji wa kutosha na kupanua biashara yake. Na mwaka wa 2003 aliweza kuwajiri wafanyi kazi wengine 10 ili kumsaidia na shughuli yake baada ya kuanzisha kampuni hiyo. Kufikia sasa, Sopey anajumla ya wafanyi kazi 20 katika kampuni yake. Kampuni hii hupata faida kutokana michezo ya kuigiza inayoandaliwa katika kumbi mbali mbali na pia kuptia michezo inayoonyeshwa moja kwa moja kupitia televisheni nchini humo inayoandika na Sopey.

**12. Atmo (pupils in rehearsal)**

**13. Narrator:**

Wanafunzi wengi humpenda sana Sopey na kutambua kazi yake.Mmoja wao ni Abdoulaye Barry. Barry ana umri wa miaka 12 na amekuwa akifanya mazoezi chini ya ukufunzi wa mkurugenzi huyu kwa muda wa miezi miwili iliyopita ili kujiandaa kwa siku ya utamaduni chuoni mwao.

**14. O-Ton: Abdoulaye Barry (fr.)**

“Tunafurahi sana kushirikiana naye. Ni Mtu mwenye ujuzi na kila mara hutupa ushauri tunaohitaji. Kwa ufupi ni mtu anayeweza kutegemewa.”

**15. Narrator:**

Marafiki zake wanaosoma pamoja chuoni pia wanavutiwa sana na ujasiri Msanii huyu.Sopey ni mpole, shupavu, lakini mwenye msimamo na kujitolea kazini. Wengi husema kuwa ni mtu mwenye masharti magumu lakini kwake hii ndio njia pekee ya kuwapa motisha wanafunzi wake.

**16. Atmo (Rehearsal going on)**

**17. Narrator:**

Sopey sasa anataka kusambaza ujuzi wake katika kila penbe ya taifa hilo. Fani hii sasa imewavutia vijana wengi wanaotaka kujiunga nayo. Sopey amekuwa kielelezo na mfano bora wa kuigwa. Yeye ni mtu wa kwanza nchini humo kuandaa michezo kutoka kwa mashairi. Ousmane Ndiaye ni mmoja wa wafanyi kazi wa Sopey na anakumbuka aliyojifunza kutoka kwake wakati walipokuwa wakiandaa mchezo wa ‘Broken Jug’ Huu ni mchezo kutoka tamthiliya iliyoandikwa na mwandishi mmoja wa vitaji wa Ujerumani Heinrich Von Kleist yapata miaka 200 iliyopita.

**18. O-Ton: Ousmane Ndiaye (fr.)**

“Nilikutana na msanii huyu mwenye kipawa miaka miwili iliyopita wakati wa tamasha kubwa lililoandaliwa mjini Dakar. Na nikamtambua kuwa ni msanii mwenye uwezo wa kutua ujumbe wa riwaya.Alitufungua macho kufahamu , na kufahamu kwamba sekta hii inaweza kukuletea pato kubwa. Wakati nilipoanza kushirikiana naye katika kutayarisha mchezo huu wa Broken Jug,nilijifunza mengi zaidi kuhusu fanihii. Hapana shaka Sopey alinisaidia sana kukuza tajriba yangu.”

**19. Narrator:**

Sopey amekuwa Mtu mashuhuri sana nchini Senegal kutokana na jinsi anavyosimamia vyema kampuni yake ya Usanii. Lakini haikuwa rahisi kufika mahali alipo .Mara nyingi alikuwa akishtumiwa na watu ambao hawakupendezwa na michezo yake,na hii ilimvuja moyo.

**20. O-Ton: Ibrahima Mbaye Sopey (fr.)**

“Tunafahamu kwamba si kila wakati mambo yanakunyokea hasa wakati unapoanzisha biashara au kitu fulani. Mwanzoni haikuwa rahisi, kwasababu wasanii mara nyingi huwapendi wasanii wageni. Mbali na hayo kuna matatizo ya kijamii, mara nyingi hupati pesa na ni lazima uende kufanya mazoezi, huku majukumu yakikusubiri nyumbani. Pia unahitaji muda wa kustarehe na marafiki, Na wakati unapokuwa na marafiki, Familia nayo inalalamika kusema huna muda tena wa kukaa nao.”

**21. Narrator:**

Lakini kwa kuzingatia mwito wake, Ujasiri na Kustahamili, hatimaye ameweza kufaulu. Mnamo mwaka wa 2003 Sopey alishiriki tamasha kubwa zaidi na kampuni yake ikashinda tuzo. Tuzo hilo sio tu lilimletea sifa bali pato kubwa pia.Sopey alitumia muda mwingi wa ujana wake kuimarisha biashara yake,na hali hii ilimfanya kukosa muda wa kuwa na familia yake. Lakini sasa ametambua umuhimu wa kuwa na familia yake na anatualika tuandamane naye hadi nyumbani kwake.

**22. Atmo: Sound effects in the district**

**23. Narrator:**

Barabara za wilaya ya Nimzat ambayo ni umbali wa Kilomita 15 kutoka Mjini Dakar ni zenye msongamano wa watu na hazipitiki kwa urahisi. Watoto wanacheza mpira mbele ya kinamama wanaouza Mboga.Wakati mmoja Sopey Sopey pia alikuwa akicheza mpira mahali hapa alipokuwa mdogo, kabla ya kuchukua jukumu la kulea familia yake akiwa na umri wa miaka 15 baada ya Babake kufariki.

**24. Atmo sound effects in the family. Sopey's mother and others members drinking tee and discussing.**

**25. Narrator:**

Nyumbani kwake anazungukwa na Dada zake, Kaka zake na mpwa, hali kadhalika Mamake ambaye amekuwa shabiki wake mkubwa siku hizi.

**26. O-Ton: Awa Mbaye (Wolof)**

"Mwanzoni sikutaka awe muigizaji. Lakini sasa nimekuwa shabiki mkubwa, ni Mtoto mzuri sana, mwenye kuishughulikia familia nzima."

**27. Narrator:**

Dadake Mdogo, Ndeye Fatou Mbaye, pia anajivunia Kakake mkubwa Sopey.

**28. O-Ton: Ndeye Fatou Mbaye (Wolof)**

"Sio tu eti ni kakangu bali rafiki mkubwa sana. Napenda kazi yake. Anafahamu vyema jinsi ya kupanga muda wake wa kazi na wakati wa kushughulikia familia, na hatuna shida tena nyumbani kila kitu tunapata".

**29. Narrator:**

Pia rafiki wa Sopey ambao hawakuwa wakimuelewa mwanzoni wanatambua juhudi zake na kumuunga mkono ingawa Sopey anakiri kuwa rahisi kuchanganya masuala ya kiuchumi na kijamii.

**30. O-Ton: Ibrahima Mbaye Sopey (fr.)**

"Kuna jambo muhimu ni kwamba matatizo yetu ya umaskini hutufanya kuwa watu wa bidii sana. Umaskini ni changamoto kubwa kwetu.Unajua ukiamuka asubuhi na huna chakula nyumbani utafanya kila juhudi kutafuta. Lakini mambo yanabadilika siku hizi. Tunaweza kujihusisha na miradi ya maendeleo, kusaidia familia zetu na kadhalika. Mfano bora wa kuigwa na vijana wengine. Hilo ni jambo linalonifurahisha sana."

**31. Narrator:**

Sopey pia alikuwa msanii mzuri sana wa televisheni nchini Senegal Watu walikuwa wakipenda sana vipindi vyake maana vilikuwa vikieleza maisha ya kawaida miongoni mwa jamii nchini humo. Na sasa ameanzisha mradi mpya wa kupambana na wizi wa hatimiliki. Hili ni jumuku muhimu zaidi kwa Sopey tangu aanzishe biashara yake.

**32.Outro:**

Na hadi hapo mpenzi msikilizaji tunafika mwisho wa kipindi hiki ambapo tumesikia mengi kuhusu juhudi za Msanii chipukizi Ibrahima Mbaye Sopey, muasisi wa kampuni ya usanii ya F'ame iliyo na makao yake mjini Dakar Senegal. Makala ya Leo ya Noa Bongo jenga maisha yako imeandikwa na Babou Diallo. Endapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki au kutuma maoni, tembelea mtandao wetu wa www.dw.de/lbe. Usikose kuungana nasi tena kwa makala nyingine wakati mwengine. Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa.